Jarida la

Ligi Kuu

Agosti 2026



www.ligikuu.co.tz



Yaliyomo

- Msimu wa Ligi 2026/2027.....2
- Pazia la Ligi Kuu ya NBC 2026/2027 lafunguliwa..... 4
- 'Wataalamu' 16 wanaosaka Taji la Ligi Kuu ya NBC 2026/2027.....5
- Nyota zao Zimeanza Kuonekana Asubuhi Ligi Kuu ya NBC.....7
- Vinara wa takwimu Ligi Kuu ya NBC 2026/2027.....9
- Jicho la Kiufundi.....11
- FVS yafungua enzi mpya ya Teknolojia soka la Tanzania.....14
- Wageni Kutoka Mali watembelea Tanzania Kujifunza.....16
- Hivi hapa viwanja vya Ligi Kuu 2026/2027.....17
- Ratiba ya NBC Championship, First League 'Yaanikwa' Kidigitali.....19
- NBC Championship 2026/2027 Kutimua Vumbi Septemba 11.....22
- Vita ya First League Kuanza Oktoba 21.....24
- Boli na Fasheni.....25







MAELEZO YA UCHAPAJI

Jarida hili huchapishwa kila mwezi na Bodi ya Ligi Kuu Tanzania - TPLB

Mhariri Mkuu
Cornel Barnabas

Mhariri Habari
Yahaya Abushehe

Mhariri Msaidizi
Honest Mwanitega

Mpiga Picha
Loveness Bernard

Msanifu Kurasa
James Onesmo

Wachangiaji
Salma Seif
Pancras Remidius
Cynthia Michael
Sakina Abdoul
Collins Mwesigwa



Bodi ya Ligi Tuu Tanzania

Ghorofa na 14, NSSF Mafao House,
Barabara ya Uhuru - Ilala,
Dar es Salaam
S. L. P 79041 Dar es Salaam

www.ligikuu.co.tz
info@ligikuu.co.tz

Ligi Kuu

ligikuu | championshiptz | firstleague

tplboard

ligikuu

Ligikuu

LIGI KUU TV

Msimu wa Ligi 2026/2027

Mwezi huu ulikuwa wa kipekee kwa kuwa uliashiria kuanza kwa Ligi Kuu ya NBC msimu wa 2026/2027, huku klabu zikirejea katika ushindani wa kutafuta ubingwa, nafasi za kimataifa na mafanikio kwa mashabiki wao. Tunatambua juhudi za klabu, wachezaji, benchi za ufundi, waamuzi, viongozi, wadau na mashabiki katika kuhakikisha msimu unaanza kwa ushindani na viwango vinavyotarajiwa.

Sambamba na kuanza kwa ligi, mwezi Agosti pia umeweka msingi wa utekelezaji wa matumizi ya teknolojia ya Football Video Support (FVS) katika mashindano yetu. Hatua hii ni sehemu ya jitihada za TFF pamoja na Bodi kuhakikisha teknolojia inatumika kuongeza usahihi wa maamuzi na kuimarisha uaminifu katika mchezo. Utekelezaji wa FVS unaendelea kwa kuzingatia taratibu na miongozo iliyowekwa, pamoja na maboresho yanayohitajika katika kipindi hiki cha utekelezaji.

Aidha, utekelezaji wa Kanuni za Mashindano umeendelea kuwa kipaumbele katika kuhakikisha ushindani unafanyika katika mazingira yenye usawa, uwajibikaji na nidhamu. Kanuni ni msingi wa uendeshaji wa mashindano na zinapaswa kuheshimiwa na kila mdau kwa nafasi yake. Bodi itaendelea kushirikiana na klabu na wadau wengine katika kutoa elimu, ufafanuzi na kusimamia utekelezaji wa kanuni hizo kwa usawa.

Katika kuendelea kutumia teknolojia kuboresha uendeshaji wa mashindano, mwezi huu pia tulishuhudia uzinduzi wa ratiba za Ligi ya Championship ya NBC na First League kupitia mfumo wa kidijitali. Hii ni hatua muhimu katika safari yetu ya kidijitali, inayolenga kufanya mchakato wa upangaji na utoaji wa ratiba kuwa wa kisasa, wenye ufanisi, uwazi na unaorahisisha upatikanaji wa taarifa kwa klabu, wadau na mashabiki.

Mafanikio haya yanaonesha dhamira yetu ya kujenga ligi inayokwenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia na mahitaji ya soka la kisasa. Hata hivyo, tunatambua kuwa safari hii ni ya pamoja. Mafanikio ya ligi yanahitaji ushirikiano wa karibu kati ya Bodi, klabu, wachezaji, waamuzi, wadau wa kibiashara, vyombo vya habari na, muhimu zaidi, mashabiki wetu.

Tunapoendelea na msimu huu, tunawahimiza wadau wote kuendelea kuzingatia nidhamu, weledi, teknolojia, uwajibikaji na uzingatiaji wa Kanuni, ili kuhakikisha tunakuwa na mashindano yenye ushindani, haki na thamani kubwa kwa soka la Tanzania.

Ninawakaribisha kusoma Jarida hili la Agosti, linalokuletea kwa kina matukio, hatua na simulizi muhimu zilizotengeneza mwanzo wa msimu wa 2026/2027.

Cornel Barnabas

Afisa Mtendaji Mkuu
Bodi ya Ligi Kuu Tanzania





PAZIA LA LIGI KUU YA NBC 2026/2027 LAFUNGULIWA

LIGI Kuu ya NBC msimu wa 2026/2027 imeanza kutimua ‘vumbi’ rasmi agosti 14 ikizikutanisha timu 16 kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania huku michezo miwili ikichezwa siku hiyo ikiwa ni baada ya mchezo wa ngao ya jamii uliozikutanisha timu za Young Africans (Bingwa wa Ligi Kuu ya NBC msimu uliopita) na Simba (Bingwa wa kombe la shirikisho la CRDB) uliochezwa katika uwanja wa Amaan Zanzibar na Young Africans kuibuka na ushindi wa bao moja.

Ikumbukwe kuwa mapema mwezi julai Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB) ilizindua ratiba ya msimu huo ikiwa ni mara ya kwanza upangaji wa ratiba hiyo kufanyika kwa mfumo wa kidijitali.

Timu zinazoshiriki Ligi Kuu ya NBC msimu wa 2026/2027 ni Azam, JKT Tanzania, Young Africans na Simba zinazowakilisha mkoa wa Dar es Salaam ambao ni mji mkuu wa kibiashara ulioko pembezoni mwa bahari ya hindi.

Fountain Gate na TRA United zikiwakilisha mkoa wa Arusha huku Polisi Tanzania iliyorejea Ligi Kuu msimu uliopita baada ya hatua ya mtoano dhidi ya Tanzania Prisons ikiwakilisha mkoa wa Kilimanjaro, Coastal Union ya Tanga ikiwa ni mikoa ya kanda ya kaskazini.

Singida Black Stars ya mkoani Singida,Dodoma Jiji ya Dodoma zikiwakilisha kanda ya kati,Pamba Jiji ya Mwanza,Geita Gold ya mkoani Geita,Kagera Sugar ya Kagera zikiwakilisha kanda ya ziwa ,Namungo ya Lindi kusini mwa nchi na Mbeya City ya Mbeya ikiwakilisha nyanda za juu kusini.

Mchezo wa kwanza wa Ligi Kuu msimu huu ulizikutanisha timu za Pamba Jiji dhidi ya Dodoma Jiji katika uwanja wa CCM Kirumba na kumalizika kwa matokeo ya 1-1 huku mchezaji wa Dodoma Jiji Berno Ngassa akifunga bao la kwanza msimu huu.

Mchezo wa pili ulizikutanisha timu za Mbeya City dhidi ya Geita Gold kwenye uwanja wa Sokoine na mabingwa wa ligi ya Championship ya NBC msimu uliopita (Geita) kupata ushindi wa bao moja ugenini huku Singida Black Stars ikiifunga Fountain Gate mabao 3-0 ikiwa ni kisasi kwa timu hiyo iliyoifunga Singida 4-3 kwenye mchezo wa mwisho wa ligi hiyo msimu uliopita.

Agosti 15 Polisi Tanzania na Azam zilikutana katika uwanja wa Sheikh Amri Abeid Arusha na mchezo huo kumalizika kwa sare ya 1-1 huku Coastal ikipoteza mchezo wake wa kwanza nyumbani kwa bao moja mbele ya Mashujaa kwenye uwanja wa CCM Mkwakwani na Namungo ilipoteza dhidi ya Young Africans katika uwanja wa Majaliwa, Lindi kwa mabao 3-1.

Mzunguko wa kwanza ulitamatika agosti 16 kwa michezo miwili ambapo Kagera Sugar iliikaribisha timu ya Simba katika uwanja wa Kaitaba na kupoteza 2-0 huku JKT Tanzania ikitoka 1-1 na TRA United.

Kuanza kwa msimu huo pia kumeenda sambamba na matumizi ya Football Video Support (FVS) katika michezo hiyo ambapo matumizi ya teknolojia hiyo yamewarahisishia waamuzi kuweza kufanya marejeo kwenye baadhi ya matukio ndani ya michezo mbalimbali ya Ligi Kuu ya NBC.

Sambamba na matumizi ya teknolojia hiyo Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) lilizindua mtandao wa manunuzi ya tiketi za michezo hiyo kupitia simu janja kwa kuingia katika tovuti ya (tff-tickets.com) na kuweza kununua tiketi ya mchezo husika wa Ligi Kuu ya NBC unaoutaka na tiketi hiyo itaskaniwa katika mageti ili kuruhusu shabiki kuingilia uwanjani.

Ligi Kuu ya NBC msimu wa 2026/2027 inatarajiwa kutamatika mei 15,2027 na ikumbukwe kuwa michezo ya mizunguko mitatu ya mwisho huwa inachezwa muda mmoja na siku moja kwa michezo yote nane na inakuwa mbashara katika chaneli mbalimbali za Azam Televisheni.



‘WATAALAMU’ 16 WANAOSAKA TAJI LA LIGI KUU YA NBC 2026/27.

LIGI Kuu ya NBC inaendelaa kukua kwa kasi kubwa ikiwaleta pamoja makocha mbalimbali wazawa na wa kigeni kufundisha timu mbali mbali za Ligi namba sita kwa ubora Afrika. Hawa hapa makocha wa timu 16 za Ligi Kuu ya NBC wanaopambana kutwaa ubingwa wa ligi hiyo msimu huu;

JEAN FLORENT IBENGE

Jean Florent Ibenge ni raia wa nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Kocha Mkuu wa timu ya Azam mwenye leseni ya CAF Pro License inayotolewa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF) akiwa na ‘wababe’ hao msimu wa pili huku akiwa amewahi kufundisha timu mbalimbali ikiwemo Al Hilal ya Sudan yenye wasifu mkubwa katika soka la Afrika na timu ya taifa ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

MANQOBA MNGQITHI

Manqoba Mngqithi ndiye Kocha Mkuu wa Mabingwa watetezi wa Ligi Kuu ya NBC timu ya Young Africans akiwa raia wa Afrika Kusini mwenye miaka 55 akimiliki leseni ya CAF A Diploma, akiwa amewahi kuzifundisha timu mbalimbali nchini kwake ikiwemo Mamelodi Sundown na Golden Arrows zinazoshiriki Ligi Kuu ya nchi hiyo.

STEVEN BARKER

Steven Barker ni raia wa Afrika Kusini mwenye miaka 58, akianza kuifundisha timu ya Simba msimu uliopita akiwa anamiliki leseni ya UEFA A na CAF Pro Licence, akiwahi kufundisha timu mbalimbali nchini kwake ikiwemo Stellenbosch na Amazulu.

HAMAD ALLY

Hamad Ally ni raia wa Tanzania na ndiye Kocha Mkuu wa timu ya JKT Tanzania akiwa na leseni ya CAF A Diploma, akipita katika timu mbalimbali ikiwemo Tanzania Prisons na KMC huku akihudumu kama kocha msaidizi wa timu ya Tanzania (Taifa Stars).

FRANCIS BARAZA

Francis Baraza ni raia wa nchi ya Kenya mwenye miaka 52 akiwa na leseni ya CAF A Diploma, anafundisha timu ya Pamba Jiji huku akiwa na ‘miamba’ hiyo ya Mwanza kwa msimu wa pili sasa na amewahi kuzifundisha Dodoma Jiji, Kagera Sugar na Biashara United.

AMANI JOSIAH

Amani Josiah ndiye Kocha Mkuu wa timu ya Mashujaa yenye maskani yake mkoani Kigoma akiwa na leseni ya CAF A Diploma, amewahi kuzifundisha timu za Dodoma Jiji na Tanzania Prisons kabla hajajiunga na ‘wazee wa mapigo na mwendo’ timu ya Mashujaa.

VICENT MASHAMI

Vicent Mashami ni raia wa Rwanda mwenye miaka 45 akiwa anamiliki leseni ya UEFA Pro, ameifundisha timu hiyo akiwa kama meneja wa timu kabla ya kusoma kozi ya refresher’s iliyoandaliwa na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) na sasa ndio Kocha Mkuu wa timu hiyo akiwa pia amewahi kuifundisha timu ya APR ya Rwanda.

ETIENNE NDAYIRAGIJE

Etienne Ndayiragije ni Kocha Mkuu wa timu ya TRA na raia wa nchi ya Burundi mwenye miaka 47 leseni ya UEFA Pro akiwa na timu ya TRA msimu wa pili sasa amewahi kuzifundisha timu za Azam, Police Kenya na nyingine nyingi.

SALUM MAYANGA

Salum Mayanga ni Kocha mtanzania mwenye miaka 58 akiwa na leseni ya CAF A Diploma, amewahi kuzifundisha timu mbalimbali ikiwemo Mashujaa na Mtibwa Sugar, huu ni msimu wake wa pili akiwa kama Kocha Mkuu wa timu ya Mbeya City.

FREDY FELIX

Fredy Felix ni Kocha Mkuu wa timu ya Fountain Gate anayemiliki leseni ya CAF A Diploma, ni raia wa Tanzania na amewahi kuzifundisha timu kama Kagera Sugar,Young Africans, Geita Gold na nyingine nyingi.

FIKIRI ELIAS

Fikiri Elias ni Kocha wa Coastal Union akiwa ni mzawa raia wa Tanzania mwenye leseni ya CAF A Diploma, amekuwa Kocha Mkuu wa timu hiyo tangu msimu uliopita na amewahi kuzifundisha JKT Oljoro na KenGold.

PAPY KIMOTO

Papy Kimoto ni Kocha mwenye miaka 50 raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) akimiliki leseni ya CAF A Diploma huku huu ukiwa ni msimu wake wa kwanza akiwa kama Kocha Mkuu wa timu ya Singida Black Stars na amewahi kuzifundisha timu za Maniema Union, JS Kinshasa na nyinginezo nyingi.

ZUBERI KATWILA

Zuberi Katwila ni raia wa Tanzania akiwa na miaka 43 anamiliki leseni ya CAF A Diploma amekuwa Kocha Mkuu wa timu ya Geita Gold tangu ikiwa Ligi ya Championship ya NBC ambapo alitwaa ubingwa msimu uliopita na amefanikiwa kuipandisha timu hiyo Ligi Kuu ya NBC, amewahi kuzifundisha pia timu za Mtibwa Sugar na Ihefu.

JUMA KASEJA

Juma Kaseja golikipa wa zamani wa timu ya Taifa ya Tanzania, ni Kocha mzawa akiwa na umri wa miaka 41 anamiliki leseni ya CAF A Diploma, ameipandisha timu ya Kagera Sugar kutoka Ligi ya Championship ya NBC hadi Ligi Kuu ya NBC msimu huu. Aliwahi kuzichezea timu za Simba na Yanga pia aliwahi kuwa Kocha msaidizi timu ya KMC.

MBWANA MAKATA

Mbwana Makata ndiye Kocha wa Polisi Tanzania aliyefanikiwa kuirejesha timu hiyo Ligi Kuu ya NBC baada ya misimu mingi kwa kucheza hatua ya mtoano dhidi ya Tanzania Prisons na kufanikiwa kuishusha daraja Prisons. Mbwana Makata anamiliki leseni ya CAF A Diploma amepita timu mbalimbali kama vile Tanzania Prisons, Mbeya Kwanza na Kagera Sugar, aidha amewahi kuwa golikipa wa timu wa Young Africans.

JUMA MGUNDA

Juma Mgunda ndiye Kocha Mkuu wa timu ya Namungo anamiliki leseni ya CAF A Diploma na ni raia wa Tanzania amecheza katika timu ya Coastal Union na kuifundisha timu hiyo pia aliwahi kuwa Kocha Mkuu wa timu ya Simba.











NYOTA ZAO ZIMEANZA KUONEKANA ASUBUHI LIGI KUU YA NBC

Msimu wa Ligi Kuu ya NBC 2026/27 bado upo katika hatua za mwanzo, lakini tayari umeanza kuwapa mashabiki picha ya nyota wanaoweza kuteka mijadala na kuwa tishio kubwa katika viwanja mbalimbali.

Baada ya raundi nne za mwanzo, kuna wachezaji walioanza kujitokeza kwa namna tofauti; wengine wakifunga mabao, wengine wakiweka rekodi na wengine wakionyesha kiwango kinachoashiria kuwa wanaweza kuwa na msimu mzuri mbele yao.

Beno Ngassa ni miongoni mwa majina yaliyoanza msimu huu kwa namna ya kipekee baada ya kuandika historia ya kufunga bao la kwanza la ligi Kuu ya NBC msimu wa 2026/27 kwenye mchezo kati ya timu yake ya Dodoma Jiji dhidi ya Pamba Jiji ugenini.

Kufunga bao la kwanza la msimu si jambo la kawaida tu, bali ni rekodi inayomweka Ngassa katika kumbukumbu ya msimu huu na bao hilo linakuwa mwanzo mzuri kwake na kumfanya kuwa mmoja wa nyota walioanza kuvuta macho ya mashabiki.

Mshambuliaji Obrey Chirwa wa Geita Gold aliyekuwa akiitumiakia Kagera Sugar msimu uliopita kwenye Ligi ya Championship ya NBC naye ameanza msimu kwa makali mbele ya lango na kujitangaza mapema katika vita ya kuwania kiatu cha ufungaji bora akiwa ndiye kinara wa mabao hadi sasa akifunga mabao manne.

Chirwa anayefahamika kwa uwezo wake wa kutafuta mabao, ameendelea kuonyesha makali yake msimu huu na kuwa miongoni mwa wachezaji wenye mwanzo bora zaidi. Kuanza kwake kwa kasi kunaashiria kuwa anaweza kuwa mmoja wa washambuliaji wa kutegemewa zaidi Geita Gold kwenye mbio za kuwania taji la Ligi Kuu ya NBC msimu huu.

Abdul Suleiman 'Sopu' wa Azam naye ameanza msimu kwa staili ya aina yake baada ya kupachika mabao manne sawa na Obrey Chirwa wakiwa vinara wa mabao. Mshambuliaji huyo tayari amefunga mabao manne katika michezo mitano, huku mabao matatu akifunga kwa mkwaju wa penati.

Uwezo wake wa kutulia na kutumia nafasi hizo umemfanya kuwa mmoja wa wachezaji walioanza vizuri zaidi. Mabao manne katika raundi tano za mwanzo ni mchango mkubwa, lakini pia yanaonyesha namna ambavyo Sopu anaweza kuwa silaha muhimu kwa Azam katika msimu huu.

Kiungo wa simba Libase Gueye,nae ni miongoni mwa wachezaji walioanza msimu wa 2026/27 kwa kiwango cha kuvutia. Gueye anaonekana kuwa silaha muhimu katika safu ya ushambuliaji ya ‘mnyama’ kutokana na uwezo wake wa kutengeneza nafasi na kutoa pasi zinazozalisha mabao.

Hadi sasa Libasse ametoa pasi tano za mabao huku akiwa amefunga bao moja na kuwa na mchango mkubwa kwenye kikosi cha Simba ambacho hadi sasa hakijapoteza mchezo wowote na kiungo huyo akihusika kwenye mabao sita kati ya tisa ambayo Simba imefunga.

Wakati huo huo, ushindani wa timu nao umeanza kutoa picha ya vita kali inayotarajiwa kuwepo kwenye mbio za ubingwa msimu huu. Mpaka kufikia raundi ya tano, ni Young Africans , Simba na Azam pekee ambazo hazijapoteza mchezo wowote wa Ligi Kuu ya NBC.

Young Africans na Simba zimeshinda michezo yote hadi sasa huku timu ya Azam ikishinda mitatu na kutoa sare miwili.

Mwanzo huo wa timu hizo tatu unaonyesha ushindani mkubwa unaotarajiwa katika msimu huu huku pia ‘wababe’ hao wakitarajiwa kupeperusha bendera ya nchi kimataifa msimu huu pamoja na timu ya Singida Black Stars.

Vinara wa takwimu Ligi Kuu ya NBC 2026/2027

Kinara wa Mabao

OBREY CHIRWA

Michezo	5
Dakika	361
Mabao	4





Kinara wa Hati safi

DJIBRILLA KASSALI

Michezo	3
Dakika	265
Hati Safi	3

Kinara wa Pasi Saidizi

LIBASE GUEYE

Michezo	5
Dakika	384
Pasi za Mabao	5





Kinara wa Kuhusika kwenye Mabao

LIBASE GUEYE

Michezo	5
Dakika	384
Mabao	1
Pasi za Mabao	5
Mabao Aliyohusika	6



Jicho la Kiufundi

Na **Sisti Martin** sistinho

WAMETISHA KWA MBINU BORA KIUZUIAJI MWEZI AGOSTI LIGI KUU YA NBC

Baada ya mechi za mwezi Agosti za Ligi kuu ya NBC, timu mbalimbali zimeonyesha ubabe wa kimbinu kwenye nyakati tofauti ndani ya dakika 90 za michezo yao na kujizolea alama nyingi kwenye msimamo wa ligi.

Kocha wa zamani wa Manchester United Sir Alex Ferguson aliwahi kunukuliwa akisema "A good Attack wins you games, a good defence wins you titles" akiwa na maana kwamba mbinu bora za kushambulia huweza kukupa ushindi lakini mbinu bora za kuzuia hukupa mataji.

Kwenye makala hii tutaona timu tatu (3) bora kwenye nyakati muhimu za kuzuia kimbinu uwanjani ambazo ni;

- Young Africans SC, mechi tano, mabao ya kufungwa mawili
- Simba SC, mechi tano, mabao ya kufungwa mawili
- Mbeya City, mechi nne, mabao ya kufungwa mawili

Timu hizi zimeonyesha kiwango kikubwa kwenye mwezi huo kwani kila timu iLiruhusu nyavu zake kutikiswa mara chache zaidi kuliko timu zote kwenye ligi katika nyakati za kuzuia zifuatazo;

Kuzuia umiliki wa mpira ukiwa kwa wapinzani (Out of Possession)

Chini ya kocha Mangqoba Mngqithi, Yanga kwenye mechi tano za mwezi huo, kati ya mabao mawili waliyofungwa, wameruhusu kufungwa bao moja pekee wakiwa kwenye umbo kamili la ulinzi huku umiliki wa mpira ukiwa kwa timu pinzani, ambapo ubora wao mkubwa ni namna wanavyoweza kuzuia kwa shinikizo kubwa kwa wapinzani wao kutokuwa huru n a kuwalazimisha kukosea hasa kwenye theluthi mbili za mwisho za uwanja (High & Mid block) wakiwa na mifumo kama 4-4-2 (diamond), 4-1-4-1 na 4-2-3-1 na kumsaidia mlinda lango wao Djigui Diarra kucheza mechi tatu akipata hati safi (Clean sheet) tatu.

Kati ya mabao mawili kwa kila timu kwenye mechi za mwezi huo, kila timu imeruhusu kufungwa bao moja lililotokana na mashambulizi ya kujibu au kushtukiza (Defensive Transitions) pindi timu hizo zinapopoteza mpira.

Chini ya kocha Steve Barker, Simba SC, kwenye mechi tano za mwezi huo, kati ya mabao mawili waliyofungwa, wameruhusu kufungwa bao moja pekee wakiwa kwenye umbo kamili la ulinzi huku umiliki wa mpira ukiwa kwa timu pinzani, ambapo ubora wao mkubwa ni namna wanavyoweza kuzuia kwa shinikizo kubwa kwa wapinzani wao kutokuwa huru na kuwalazimisha kukosea hasa kwenye theluthi mbili za mwisho za uwanja (High & Mid block) wakiwa na mifumo kama 4-3-3, 4-2-3-1 huku wakimsaidia mlinda lango wao kupata hati safi kwenye mechi tatu (Clean Sheet).

Chini ya kocha Salum Mayanga, Mbeya City, kwenye mechi zao nne za mwezi huo, kati ya mabao mawili waliyofungwa, wameruhusu kufungwa bao moja pekee wakiwa kwenye umbo lao kamili la ulinzi huku umiliki wa mpira ukiwa kwa timu pinzani, kama ilivyokuwa kwa Simba SC na Yanga SC, ambapo ubora wao mkubwa ulikuwa namna walivyo na ukuta usiopitika kirahisi kwenye theluthi zote za uwanja na wachezaji wao wakijitahidi kujitoa kushinda kila pambano uwanjani na kumlinda mlinda lango wao kupata hati safi kwenye michezo mitatu (clean Sheet).







Timu hizi zote zimekuwa na wastani mzuri wa kuzuia mashambulizi ya kujibu yanayotokea sekunde chache baada ya kupoteza umiliki wa mpira kabla hawajarejea kwenye muundo wao kamili wa kuzuia, na hapo silaha zao kuu zilikuwa;

(i) Kuzuia kwa haraka pale wanapopoteza mpira (Counter Pressing), mfano ni mistari wa mbele wa wachezaji wa Yanga, Shalulile, Toure wakifuatiwa na Maxi , Kangwanda na Mudathir wanavyoanza kuzuia haraka pindi wanapopoteza mpira

(ii) Kuwa na umbo bora kwenye mistari miwili ya nyuma timu ikiwa na mpira kwenye nusu ya wapinzani ambalo linaweza kumeza shambulizi la kujibu pindi wachezaji wa mbele wanapopoteza mpira (Rest Defence), mfano ni umbo la 3-2 (kwenye muundo wa 3-2-5) linaloundwa na Simba ambapo mstari wa nyuma huwa na Rushine, Toure na Mbegu na mbele yao Chilambo na Maema.

(iii) Wachezaji kurejea kwa haraka kwenye maeneo sahihi ili kurejesha umbo la kuzuia kabla hawajaathiriwa na mashambulizi ya kujibu ya wapinzani (Recovery Runs) mfano ni Mbeya City, pindi wachezaji wao wa mbele wanapopoteza mpira hurejea haraka kwenye maeneo wanayopaswa kuwepo kulingana na mfumo wa timu ambao mara nyingi ni 4-4-2 na mara nyingi wachezaji wao wa pembeni Willy Mwani na Eliud Ambokile hukimbia haraka kurejea kwenye mstari sawa na viungo Adily Buha na Omar Hamis ili kutoruhusu mabeki wa pembeni, Jimson Mwanuke na Yahya Mbegu kutozidiwa idadi na wapinzani.

Hizo zimekuwa nguzo zao tatu muhimu za kimbinu kuweza kuzuia mashambulizi ya kujibu kuweza kuwaathiri pindi wachezaji wanapopoteza mpira hasa kwenye nusu ya mpinzani.

Kutokana na mbinu bora za kuzuia timu hizo zimeweza kutumia uzuiaji wao bora kuweza kuzaa mabao kwa kutumia mashambulizi ya kujibu (Offensive Transitions), nyakati ambazo huzuia vizuri njia za wapinzani wao kupita au kuwashinikiza kukosa na kupora mipira na kujibu mashambulizi kabla wapinzani hawajarejea kwenye miundo yao ya kuzuia.

Hii ni mifano ya mabao yao yaliyotokana na uzuiaji bora;

Yanga SC, kati ya mabao 15 waliyofunga hadi sasa, mabao matano yametokana na mashambulizi ya kujibu baada ya kupora mpira, mfano bao la tatu walilofunga kwenye mchezo dhidi ya Namungo ambapo Yanga wakiwa na muundo wa 4-1-4-1, walianza kuzuia kwa shinikizo kubwa shambulizi la Namungo waliloanza kulijenga kuanzia kwenye theluthi yao ya kwanza ya uwanja, mstari wa kwanza wa uzuiaji wa Yanga ulikuwa na Peter Shalulile dhidi ya mabeki wa kati wa Namungo huku nyuma yake kukiwa na Maxi na Mudathir dhidi ya viungo wa kati wa Namungo na Kangwanda na Zokuani dhidi ya mabeki wa pembeni wa Namungo baada ya shinikizo kubwa lililowekwa na Zokuani kwa beki wa kulia wa Namungo, beki huyo alilazimika kurejesha mpira nyuma ukanaswa na Shalulile ambaye aliweza kufunga.

Simba SC, kati ya mabao tisa waliyofunga, mabao mawili yametokana na mashambulizi ya kujibu baada ya kupora mpira, mfano ni bao la pili walilofunga kwenye mchezo dhidi ya Geita Gold ambapo Simba wakiwa kwenye muundo wao wa 4-4-2, walitengeneza ukuta unaozuia njia za Geita kuweza kupenya na kutengeneza nafasi kwenye theluthi yao ya mwisho kuzuia kabla ya lango lao kufikiwa, Chilambo akiwa kwenye mstari wa mabeki wanne wa nyuma ananasa pasi ya beki wa pembeni wa Geita Gold Martin Kigi na kuanzisha shambulizi la kujibu ambalo alipiga pasi ya haraka kwa Anicet Oura akiwa sambamba na mabeki wa kati wa Geita ambaye aliunganisha kwa Elie Mpanzu aliyeshambulia nafasi pembeni na kufungua njia kwenye nusu nafasi (half space) iliyochukuliwa na Chilambo tena kwenye boksi aliyepiga krosi kisha Libasse Gueye akamalizia kwa urahisi.

Mbeya City FC, Kati ya mabao sita waliyofunga, mabao manne yametokana na mashambulizi ya kujibu baada ya kupora mpira, mfano ni bao la pili walilofunga kwenye mchezo dhidi ya Fountain Gate ambapo wakiwa wamezuia vizuri na muundo wa 5-4-1 (baada ya mabadiliko kipindi cha pili) na kumsimamisha Oscar Mwajanga peke yake mbele, Omar Hamis akiwa kwenye mstari wa viungo wanne anapora mpira kutoka kwa kiungo wa Fountain Gate na kupiga pasi mpenyezo kwa Oscar Mwajanga aliyekuwa ameshambulia nafasi nyuma ya mabeki wa Fountain Gate na kuweza kufunga bao.

Hadi sasa timu hizo zimetengeneza wastani mzuri wa mabao kutokana na uzuiaji wao bora ikiwa ni silaha yao kuu iliyowasaidia kuwa na alama nyingi kwenye mechi za mwezi Agosti.

FVS YAFUNGUA ENZI MPYA YA TEKNOLOJIA SOKA LA TANZANIA



Ligi Kuu ya NBC na soka la Tanzania limeandika historiampya katika historia ya soka nchini baada ya kuanza rasmi kutumia teknolojia ya Football Video Support (FVS), hatua inayolenga kuongeza usahihi wa maamuzi na kuimarisha haki ndani ya michezo.

Matumizi ya teknolojia hiyo yalianza rasmi Ijumaa, Agosti 14, 2026, siku ambayo msimu mpya wa Ligi Kuu ya NBC 2026/27 ulifunguliwa kwa mchezo kati ya Pamba Jiji na Dodoma Jiji katika Uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza.

Mchezo huo uliomalizika kwa sare ya bao 1-1, haukuwa tu mwanzo wa msimu mpya wa ligi, bali pia uliingia kwenye historia kama moja ya matukio muhimu katika safari ya maendeleo ya soka Tanzania baada ya kuwa mchezo wa kwanza kushuhudia matumizi ya Football Video Support (FVS) katika Ligi Kuu ya NBC.

FVS ni teknolojia inayompa mwamuzi msaada wa kupitia upya baadhi ya matukio muhimu yenye mashaka ambayo yanaweza kuwa na athari kubwa katika matokeo ya mchezo. Teknolojia hiyo inalenga kusaidia kufanya maamuzi sahihi katika matukio kama mabao, penalti, kuotea na matukio mengine muhimu yanayohitaji marejeo.

Katika mchezo wa Pamba Jiji dhidi ya Dodoma Jiji, teknolojia hiyo ilianza kuonesha umuhimu wake pale lilipotokea tukio lililohitaji marejeo. Baada ya Pamba Jiji kupata bao la kusawazisha kupitia Deogratius Judika Mafie, upande wa Dodoma Jiji uliwasilisha ombi la tukio hilo kupitiwa kwa kutumia FVS na baada ya marejeo kufanyika, ilibainika kuwa bao hilo lilikuwa halali na uamuzi wa mwamuzi ukaendelea kusimama.

Hali hiyo ilitoa picha ya kwanza kwa mashabiki, wachezaji, makocha na wadau wa soka kuhusu namna teknolojia hiyo itakavyokuwa sehemu ya mchezo katika msimu wa 2026/27.

Tofauti na mfumo wa VAR ambao hutegemea waamuzi wa video kufuatilia matukio kwa mfumo maalumu, FVS inatoa nafasi kwa benchi la ufundi kuomba marejeo ya matukio muhimu kwa kufuata taratibu zilizowekwa huku uamuzi wa mwisho ukiendelea kubaki mikononi mwa mwamuzi wa mchezo.

Kuanzishwa kwa FVS kunatajwa kama hatua kubwa katika safari ya soka la Tanzania kuelekea matumizi makubwa ya teknolojia, hasa katika kipindi ambacho ushindani wa Ligi Kuu ya NBC unaendelea kukua na kila uamuzi unaweza kuwa na mchango mkubwa katika matokeo ya timu.

Kwa mashabiki, teknolojia hiyo inatarajiwa kuongeza imani katika maamuzi ya waamuzi, huku kwa waamuzi wenyewe ikiwa ni nyenzo muhimu ya kuwasaidia katika matukio ambayo kasi ya mchezo inaweza kufanya iwe vigumu kuyaona kwa usahihi.

Hata hivyo, matumizi ya FVS pia yanahitaji uelewa mkubwa wa kanuni zake. Kwa mujibu wa taratibu za ligi, ni Kocha Mkuu au kiongozi mwingine wa juu wa benchi la ufundi mwenye mamlaka ya kuwasilisha ombi la marejeo, huku wachezaji wakitakiwa kufuata utaratibu huo badala ya kumshinikiza moja kwa moja mwamuzi.

WAGENI KUTOKA MALI WATEMBELEA TANZANIA KUJIFUNZA.

Tanzania imeendelea kuwa kitovu muhimu cha kujifunza na kubadilishana uzoefu katika maendeleo na uendeshaji wa soka barani Afrika, baada ya wawakilishi kutoka Shirikisho la Soka Mali, Abidane Issa Sangare na Niama Loua Berette kufanya ziara maalumu ya kujifunza mifumo mbalimbali ya uendeshaji wa soka nchini Agosti 25, 2026.

Ziara hiyo ililenga kuwawezesha wageni hao kupata uelewa mpana kuhusu namna soka linavyosimamiwa, kuendeshwa na kuendelezwa Tanzania, kuanzia ngazi ya shirikisho, bodi ya ligi hadi kwenye uendeshaji wa klabu.

Wageni hao walifika ofisi za Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) na Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB) ambapo walipata fursa ya kujifunza kuhusu mifumo ya uendeshaji wa mpira, usimamizi wa mashindano, maendeleo ya soka, uratibu wa michezo pamoja na majukumu mbalimbali yanayotekelezwa na Shirikisho katika kuhakikisha mchezo unaendelea kukua nchini.

Ziara hiyo ilitoa nafasi pia kwa pande hizo kubadilishana uzoefu, changamoto na mbinu mbalimbali zinazoweza kusaidia kuimarisha maendeleo ya soka katika taifa lao.

Ziara hiyo iliendelea katika ngazi ya klabu, ambapo wageni hao walitembelea timu ya Azam na kupata fursa ya kujifunza namna klabu hiyo inavyoendesha shughuli zake ambapo kikao hicho walifanya na mwenyeji wao Afisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo Octavi Anoro.

Walipata nafasi ya kuona kwa karibu mifumo ya uendeshaji wa klabu, mipango ya maendeleo na namna shughuli mbalimbali zinavyounganishwa katika kujenga taasisi ya kisoka yenye ushindani.

Aidha, walitembelea klabu ya Young Africans katika ofisi za klabu hiyo, ambako walipata fursa ya kujifunza zaidi kuhusu uendeshaji wa klabu hiyo, usimamizi wa shughuli zake na namna klabu inavyoshirikiana na wadau mbalimbali katika kukuza thamani na mafanikio ya taasisi ambapo walikuwa na Afisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo Andrea Mtine pamoja na viongozi wengine wa timu hiyo.

“Shirikisho letu liliona kuna umuhimu wa kukuza namna yetu ya kuendesha soka letu, hivyo tukaamua kufuata misingi ambayo Tanzania inatumia kwani ni moja ya sehemu iliyoendelea kwenye soka, hii ndiyo sababu kuu ya sisi kuja kujifunza” Alisema Niama Berette.

Moja ya sehemu muhimu zaidi ya ziara hiyo ilikuwa ni kupata nafasi ya kushuhudia kwa vitendo namna siku ya mchezo inavyoendeshwa.

Hilo lilikamilika kwenye Uwanja wa Mej. Isamuhyo, Dar es Salaam na kushuhudia mchezo wa Simba dhidi ya Coastal Union, ambapo walipata fursa ya kuona kwa karibu maandalizi na utekelezaji wa shughuli mbalimbali zinazohusiana na siku ya mechi.

Kutazama mchezo huo kulikuwa sehemu muhimu ya safari yao ya kujifunza, kwani waliweza kuunganisha maarifa waliyoyapata kwenye ofisi za taasisi na klabu na kile kinachotokea uwanjani wakati mashindano yakiendelea.

Kwa ujumla, ziara hiyo imekuwa darasa muhimu la kubadilishana uzoefu kati ya Tanzania na Mali, likionyesha umuhimu wa mataifa ya Afrika kujifunza kutoka kwa kila mmoja katika kuendeleza sekta ya michezo.

Ziara hiyo pia imeonyesha kuwa maendeleo ya soka Afrika hayaishii kwenye uwanja pekee. Yanahitaji mifumo imara ya uendeshaji, taasisi zenye uwezo, klabu zinazojengwa kitaalamu, ligi zinazosimamiwa kwa ufanisi na ushirikiano wa karibu kati ya wadau.



HIVI HAPA VIWANJA VYA LIGI KUU 2026/2027

KAITABA - KAGERA
Ni uwanja wa nyasi bandia uliopo katika mkoa wa Kagera, ndipo nyumbani kwa timu ya Kagera Sugar iliyopanda daraja msimu huu baada ya kumaliza nafasi ya pili na timu hiyo imechagua uwanja wa CCM Kirumba kama uwanja wa mbadala wa timu hiyo huku ikitumia Kaitaba kama uwanja wa mazoezi..

CCM KIRUMBA-MWANZA
Ni uwanja wa nyasi asilia uliopo eneo la Kirumba jijini Mwanza ambapo ndio nyumbani kwa timu ya Pamba Jiji maarufu kama (TP Lindanda) na timu hiyo itatumia uwanja wa Nyamagana kama uwanja mbadala huku mazoezi wakifanya katika uwanja wa chuo cha ualimu Butimba.

LAKE TANGANYIKA-KIGOMA
Uwanja wa nyasi asilia uliopo mkoani Kigoma na ndio uwanja wa nyumbani wa timu ya Mashujaa huku timu hiyo ikichagua uwanja wa Jamhuri, Dodoma kama uwanja mbadala na Bulonge utakuwa uwanja wao wa mazoezi.

BUKOMBE-GEITA
Ni uwanja mpya wa nyasi bandia uliopo Bukombe mkoani Geita, ndipo patakuwa nyumbani kwa ‘wachimba dhahabu’ Geita Gold huku wakichagua uwanja wa CCM Kirumba kama uwanja mbadala na mazoezi watakuwa wakifanya katika uwanja wa Shule ya Waja

AIRTEL -SINGIDA
Uwanja huo wa nyasi bandia upo mkoani Singida ndio watakaotumia wababe wa Singida Black Stars kama uwanja wao wa nyumbani na uwanja mbadala wa timu hiyo utakuwa uwanja wa Liti uliopo mkoani humo na mazoezi watafanya katika uwanja wao wa Airtel.

SOKOINE -MBEYA
Ni uwanja wa nyasi asilia nyumbani kwa timu ya Mbeya City, upo katika jiji la Mbeya na aidha timu hiyo imechagua uwanja wa Tanzanite Kwaraa uliopo Babati Manyara kama uwanja mbadala na mazoezi ya timu hiyo itakuwa ikifanya katika uwanja wa Isesye jijini Mbeya

.



JAMHURI-DODOMA
Uwanja huo wa nyasi asilia upo makao makuu ya nchi yaani Dodoma ndio uwanja wa nyumbani wa timu ya Dodoma Jiji huku timu hiyo ikichagua uwanja wa Airtel kama uwanja mbadala na kwenye mazoezi timu hiyo itafanya katika uwanja wa John Merlin mkoani Dodoma.

.

MAJALIWA -LINDI
Hapa ni nyumbani kwa ‘wauaji wa kusini’ yaani timu ya Namungo, uwanja huo wa nyasi bandia upo Ruangwa, Lindi ambapo timu hiyo pia itatumia uwanja wa Ilulu kama uwanja mbadala huku mazoezi itakuwa ikifanya katika uwanja wa shule ya Wonder Kids

SHEIKH AMRI ABEID-ARUSHA
Uwanja huo wa nyasi asilia uliopo kaskazini mwa Tanzania mkoani Arusha ambapo utakuwa uwanja wa nyumbani wa timu za TRA United, Fountain Gate na Polisi Tanzania huku timu hizo zikichagua uwanja wa Black Rhino uliopo Karatu mkoani humo kama uwanja mbadala na TRA watafanya mazoezi katika uwanja wa Aga Khan mkoani hapo.

MKWAKWANI -TANGA
Ni uwanja wa nyasi asilia uliopo mkoani Tanga ambapo ndio nyumbani kwa timu ya Coastal Union ya mkoani humo na mazoezi watafanya katika uwanja huo huo.

MEJA JENERALI ISAMUHYO-DAR ES SALAAM
Ni uwanja wa nyasi asilia na nyumbani wa timu ya JKT Tanzania na timu ya Simba unapatikana Mbweni mkoani Dar es Salaam huku timu hizo zikichagua kutumia uwanja wa KMC Complex kama uwanja mbadala na mazooezi JKT watafanya katika uwanja wao wa Meja Jenerali Isamuhyo huku timu ya Simba ikifanya katika uwanja wake wa Mo Arena ..

AZAM COMPLEX-DAR ES SALAAM
Ni uwanja nyasi bandia uliopo jijini Dar es Salaam wenye kukadiriwa kubeba mashabiki zaidi ya 6000, utakuwa uwanja wa nyumbani wa timu ya Azam huku uwanja wa KMC Complex uliopo Mwenge mkoani Dar es Salaam ukitumika kama uwanja mbadala wa timu hiyo na mazoezi wakifanya katika uwanja wao wa Azam Complex.

UHURU-DAR ES SALAAM
Ni uwanja wa nyasi bandia uliopo mkoani Dar es Salaam ambao utakuwa nyumbani kwa ‘vigogo’ wa Ligi Kuu ya NBC yaani Simba na Young Africans huku timu hizo zikitumia uwanja wa KMC kama uwanja mbadala na mazoezi Simba itafanya uwanja wa Mo Arena na Young Africans ikifanya uwanja wa Avic Town.

KMC COMPLEX - DAR ES SALAAM
Ni uwanja wa nyasi bandia uliopo Mwenge mkoani Dar es Salaam ndio nyumbani kwa Young Africans huku timu hiyo ikitumia uwanja wa Uhuru kama uwanja mbadala na mazoezi timu hiyo ya Young Africans ikifanya uwanja wa Avic Town

RATIBA NBC CHAMPIONSHIP, FIRST LEAGUE 'YAANIKWA' KIDIJITALI.

AGOSTI 28, 2026 Soka la Tanzania liliandika ukurasa mwingine muhimu katika safari yake ya maendeleo baada ya ratiba za Ligi ya NBC Championship na First League kuzinduliwa kidijitali kwa mara ya kwanza, katika hafla iliyofanyika kwenye ukumbi wa Hoteli ya Johari Rotana, Dar es Salaam.

Uzinduzi huo wa kihistoria umeashiria mwelekeo mpya wa namna mashindano ya mpira wa miguu nchini yanavyoendelea kusimamiwa, kutangazwa na kusogezwa karibu zaidi na wadau kupitia matumizi ya teknolojia na majukwaa ya kidijitali.

Kwa mara ya kwanza, wadau wa soka, viongozi wa klabu, mashabiki na vyombo vya habari wamepata fursa ya kushuhudia ratiba za ligi hizo zikitambulishwa kwa mfumo wa kisasa wa kidijitali, hatua inayodhihirisha dhamira ya kuendana na kasi ya mabadiliko ya dunia ya michezo.

Tukio hilo halikuwa tu uzinduzi wa ratiba bali pia lilitoa picha ya mabadiliko makubwa yanayoendelea katika soka la Tanzania. Katika dunia ya sasa, teknolojia imekuwa sehemu muhimu ya ukuaji wa michezo, kuanzia namna taarifa zinavyowafikia mashabiki, uuzaji wa bidhaa za ligi, matangazo, uchambuzi wa takwimu hadi ujenzi wa mahusiano makubwa kati ya waendeshaji wa mashindano na wadhamini.

NBC Championship, ambayo imeendelea kuwa moja ya mashindano muhimu katika mfumo wa maendeleo ya soka Tanzania, inatoa jukwaa kubwa kwa klabu na wachezaji kupambana kuelekea Ligi Kuu ya NBC. Kwa upande wa First League, mashindano hayo yanaendelea kuwa sehemu muhimu ya kukuza vipaji, kuimarisha ushindani na kutoa fursa kwa klabu kutoka maeneo mbalimbali nchini huku timu zake zikisaka fursa ya kupanda Ligi ya Championship ya NBC.



Hatua ya kuzindua ratiba hizi kidijitali pia inafungua milango kwa fursa mpya za kibiashara na kimkakati. Kadiri mashindano yanavyozidi kuratibiwa kisasa, kuonekana na kufuatiliwa kupitia majukwaa mbalimbali ya kidijitali, ndivyo thamani ya ligi, klabu, wachezaji na wadhamini inavyoweza kuongezeka.

Kwa soka la Tanzania kwa ujumla, uzinduzi huu unawakilisha jambo kubwa zaidi ambalo ni dhamira ya kujenga mfumo wa soka unaokwenda sambamba na maendeleo ya teknolojia na mahitaji ya kizazi cha sasa.

Tukio la Agosti 28, 2026, linabaki kuwa alama muhimu katika historia ya mashindano ya NBC Championship na First League kwani kadiri teknolojia inavyoendelea kubadilisha namna dunia inavyoendesha na kufuatilia michezo, soka la Tanzania nalo linaendelea kupiga hatua mbele.





NBC CHAMPIONSHIP 2026/27 KUTIMUA VUMBI SEPTEMBA 11

BAADA Geita Gold, Kagera Sugar na Polisi Tanzania kufanikiwa kuhitimisha safari yao ya kupanda Ligi Kuu ya NBC, sasa macho ya mashabiki wa soka nchini yanaelekezwa kwenye msimu mpya wa NBC Championship 2026/27 utakaoanza Septemba 11, 2026, ambapo vita nyingine ya kusaka tiketi za kupanda daraja itaanza.

Geita Gold walimaliza msimu uliopita wakiwa mabingwa wa NBC Championship baada ya kukusanya alama 77, huku Kagera Sugar wakimaliza nafasi ya pili kwa alama 72, matokeo yaliyowapa nafasi ya kupanda Ligi Kuu ya NBC. Polisi Tanzania nao walifanikiwa kuondoka Championship baada ya kuifunga Prisons kwenye matokeo ya jumla ya hatua ya mtoano.

Msimu wa 2026/27 sasa unazikutanisha timu zenye historia, uzoefu na malengo tofauti, huku kila mmoja akitazama nafasi ya kutumia ushindani huo kama daraja la kuelekea Ligi Kuu.

Timu zitakazoshiriki katika msimu huu ni Rhino Rangers, KMC, Kengold, Kigamboni United, Stand United, IAA, Transit Camp, Songea United, Tanzania Prisons, Mbuni , Bigman , Mtibwa Sugar, Gunners , Mbeya Kwanza, TMA na Bandari Tanzania, ikikamilisha idadi ya washiriki 16 wa msimu mpya.

Mtibwa Sugar, Tanzania Prisons na KMC ni miongoni mwa timu zitakazoingia kwenye msimu huu zikiwa na uzoefu wa kucheza Ligi Kuu ya NBC. Historia yao inaweza kuwa silaha muhimu, lakini uzoefu pekee hautatosha katika ligi inayohitaji matokeo ya ushindi wa mara kwa mara kwa msimu mzima.

Kwa Mbeya Kwanza, Transit Camp na Stand United, msimu huu unatoa nafasi nyingine ya kuonyesha ubora na kupambana kwa ajili ya nafasi za juu kwani ni timu ambazo zimekuwa zikishiriki ligi hii mara kwa mara. Ushindani unatarajiwa kuwa mkubwa kuanzia mwanzo wa msimu, huku kila timu ikitafuta mwanzo mzuri wa kujijengea mazingira ya kuwa na safari ya mafanikio.

Kengold, Kigamboni United, Songea United, Mbuni FC, Bigman FC na Gunners nazo haziwezi kupuuzwa kwenye mbio za ubingwa wa NBC Championship msimu huu zikiwa na uzoefu wa kushiriki ligi hiyo msimu uliopita, ambapo zinaweza kufaidika na uzoefu huo kwa kuelewa kuwa tofauti ya alama chache inaweza kubadilisha nafasi ya timu kwenye msimamo na kufanya kila mchezo kuwa wa umuhimu mkubwa.

Mbali na vita ya kupanda daraja, NBC Championship pia inatarajiwa kuendelea kuwa jukwaa la kuibua vipaji vipya. Wachezaji watautumia msimu huo kujitangaza na kuonyesha uwezo wao, huku wengine wakitafuta nafasi ya kuvutia macho ya timu kubwa na wadau wa soka nchini.

Je, ni timu gani itatumia uzoefu na nafasi itakazopata kutwaa ubingwa au kurejea kwenye Ligi Kuu ya NBC msimu ujao? Majibu ya maswali hayo yatapatikana uwanjani kadri msimu utakavyoendelea, lakini kwa sasa, jambo moja linaonekana wazi NBC Championship 2026/27 inakwenda kuwa vita ya alama, ushindani na ndoto ya kufuata nyayo za Geita Gold, Kagera Sugar na Polisi Tanzania kuelekea Ligi Kuu ya NBC.





Wachezaji wa timu za KMC (kushoto) na Bandari (kulia) wakifanya mazoezi kujiandaa na Ligi ya Championship ya NBC inayotarajia kuanza September 11, 2026

‘VITA’ YA FIRST LEAGUE KUANZA OKTOBA, 21.

LIGI ya First League inatarajia kuanza octoba 21, 2026 ikiwa ni msimu wa 2026/2027 wa ligi hiyo ambayo itazikutanisha timu 16 ambazo zitagawanywa katika makundi mawili ili kupata timu mbili vinara zitakazopanda Ligi ya Championship ya NBC.

Kundi A la Ligi ya First League litakuwa na timu za Hausung ya mkoani Njombe, Barberian, Magnet, Pan African, Cosmopolitan na Dar City zikiwakilisha mkoa wa Dar es Salaam, Nyumbu ya Pwani huku Moro Kids ikiwakilisha mkoa wa Morogoro.

Kundi B litazikutanisha timu za Alliance na Copco za mkoani Mwanza, Madini ya Shinyanga, Kigoma FC ya mkoani Kigoma, Endument ya mkoani Kilimanjaro, Mt Hanang ya Manyara,African Sport na NKIM za mkoani Tanga.

Michezo ya kwanza kwa timu za kundi A ni Hausang dhidi ya Barberian katika uwanja wa Amaan, Njombe,Magnet dhidi ya Nyumbu uwanja wa Filbert Bayi, Pwani,Cosmopolitan dhidi ya Pan Africans uwanja wa Jamhuri Morogoro na Dar City dhidi ya Moro Kids katika uwanja wa Jamhuri Morogoro.

Kwa upande wa Kundi B michezo ya mzunguko wa kwanza itakuwa ni Alliance dhidi ya Madini United uwanja wa Nyamagana,Kigoma Fc dhidi ya Mt Hanang katika uwanja wa Lake Tanganyika, NKIM dhidi ya Africans Sport uwanja wa Mkwakwani Tanga na Copco dhidi ya Endument katika uwanja wa Nyamagana.

Aidha Ligi hiyo inatarajia kutamatika machi 28,2026 ambapo vinara wa kila kundi watawaeza kupanda daraja kwenda Ligi ya Championship ya NBC huku timu zizazoshika nafasi ya pili na tatu zikicheza hatua ya mtoano wa kufuzu kwenda kucheza na timu ya Championship iliyopo katika hatua ya mtoano.



Wachezaji wa Nyumbu FC wakiendelea na mazoezi kujiandaa na msimu wa First League 2026/27

‘BOLI’ & ‘FASHENI’

Aboutwalb Mshery

Amani Josiah

TUNAKUONA MBALI TAJIRI

NBC
Benki ya Taifa ya Biashara
Daima Karibu Nawe.

Lipa Kibingwa Ukiwa Popote

Fanya malipo kupitia Lipa Kiganjani kwa Kuscan QR au Lipa Namba ya mtandao wowote.



Piga ***150*55#** au Pakua App ya **NBC Kiganjani** PlayStore au AppStore